



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**  
**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MKUTANO WA WADAU WA RELI, TIKETI MTANDAO NA MAZUNGUMZO  
KUHUSU TEKSI MTANDAO**

**1. MKUTANO WA WADAU WA RELI**

- Tumepokea maombi ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) ya kufanya mapitio ya nauli za treni
- Tumeandaa vikao na wadau – Dar (19/08/2022), Arusha (13/09/2022 – Police Mess), Mwanza (16/09/2022 – Jiji la Mwanza) na Kigoma (20/09/2022-Kigoma Social Hall).
- Tunawakaribisha wadau

**2. TIKETI MTANDAO**

- Mwisho wa utekelezaji ulikuwa 31/08/2021 – Mwitikio ni mzuri kwa wenye mabasi wengi. Mabasi yote ya masafa marefu yameshajiunga
- Tunawashukuru sana wamiliki wa mabasi na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), pia watoa huduma za tiketi mtandao (vendors) kwa hatua hii. Haturudi nyuma, tunaendelea kuboresha mapungufu yaliyojitokeza.
- Zipo changamoto ambazo hasa kinacodaiwa ni kukosekana kwa mtandao – hili tuliamini lisingekuwepo endapo wamiliki wote wangeingiza mabasi yao kwenye Mfumo Jumuishi wa Mauzo ya Tiketi (Universal Ticketing System) ambapo abiria watakuwa wanachagua mabasi wenyewe popote walipo, watachagua kiti na kujikatia tiketi wenyewe.
- Niwasihi na kuwasisitiza ‘vendors’ wahakikishe mifumo yao imeungwa kwenye mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Tulishatoa muda wa mwisho na wale ambayo watakuwa hawajiunga kufikia tarehe 30 Septemba 2022 tutataka maelezo kwanini tusiwatoe kwenye huduma hii.
- Kwa hatua tuliyofikia, tunahitaji zaidi kukaa pamoja kila mara na wadau wetu kufanya tathmini na kutatua changamoto zinazojitokeza.

### 3. MAZUNGUMZO NA BOLT/UBER

Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kwa mujibu wa Sheria Na. 3 ya mwaka 2019 ilitangaza viwango vya nauli za tekisi mtandao kupitia Gazeti la Serikali Na. 1369 la tarehe 8 Aprili, 2022 na vyombo vingine vya habari.

Aidha, kampuni za mifumo ya tekisi mtandao za Bolt na Uber zilisitisha baadhi ya huduma za usafiri wa tekisi mtandao kufuatia kutoridhika na kiwango cha ukomo cha kamisheni cha asilimia 15 wanayopaswa kuwatoza madereva husika.

Mamlaka inaendelea kushughulikia changamoto za huduma za tekisi mtandao, ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na madereva na kampuni za tekisi mtandao nchini.

Kati ya tarehe 5 na 8 Septemba, 2022, Mamlaka ilifanya vikao na Chama cha Madereva wa Tekisi Mtandao Tanzania (TODA), kampuni za Bolt na Uber ili kubadilishana taarifa na hoja za kibiashara na kiuchumi ili kusaidia kampuni za mifumo ya tekisi mtandao, madereva na abiria kupata huduma bora, endelevu na kwa thamani halisi ya pesa.

Kufuatia vikao hivyo, Mamlaka imeona itoe taarifa kwa umma kwamba vikao vyetu na mazungumzo yetu na TODA, Bolt na Uber yalikuwenda vizuri. Kuna taarifa ya maandishi tunasubiri tupate leo na si Zaidi ya kesho toka kwa Bolt na Uber ili na sisi tukamilishe taratibu zetu za ndani kabla hatujatangaza rasmi maamuzi ya Mamlaka.

Niwashukuru kipekee Uongozi wa TODA na watoa huduma wa tekisi mtandao walioendelea kutoa huduma ikiwa ni pamoja na Paisha, Ping, Indrive na Little Ride.

Asanteni Sana kwa kunisikiliza.

**Imetolewa na;**

**CPA HABIBU J. S. SULUO**  
**Mkurugenzi Mkuu**  
**Tarehe 12 Septemba, 2022**

